

## 2. Kumwona daktari

### Daktari mkuu

- Nchini Australia watu wengi huenda kwa daktari wa familia wakati wana shida ya afya au wanapo hitaji kuangaliwa kiafya. Madaktari wa familia pia wanajulikana kama 'madaktari wa kijumla' (GP)
- madaktari wa familia huangalia afya yako kwa ujumla ya kimwili na matukutiko yoyote ya ki-afya. Madaktari hawa ni watu wa kwanza ambao watu wengi huwaendea kwa shida ya kiafya, isipokuwa katika wakati wa dharura.
- madaktari wa familia wataamua ikiwa unahitaji vipimo vyovyote, kumwona mtaalamu, kuenda hospitali au ikiwa wanaweza kutibu shida yako ya afya hapo kwa hapo.
- madaktari wa familia hufanya kazi katika ofisi ndogo au kliniki zinazoitwa 'medical centres' (vituo vya matibabu) au 'surgeries' (vyumba vya upasuaji). Mengi ya vituo hivi hufunguliwa kutoka saa tatu asubuhi hadi saa kumi na moja jioni kutoka Jumatatu hadi Ijumaa. Baadhi zao hufunguliwa kwa masaa mengi pamoja na mwisho wa wiki. Kuna vituo vichache vinvofunguliwa kwa masaa 24 kwa siku.
- una uhuru wa kumchagua daktari wako wa familia. Ni muhimu uwe umeridhika na daktari wako wa familia. Kama hujaridhika, una uhuru wa kumchagua daktari mwingine.
- ni ubora kuwauliza marafiki, familia au watu katika jamii yako kuhusu mapendekezo ya daktari wa familia ambaye anafahamu kutumia wakalimani au anaye zungumza lugha yako. Kama sivyo, angalia katika kurasa za manjano ya shirika la simu (yellow pages) chini ya 'medical practitioners' (madaktari wa matibabu).



Interpreter

### Wakalimani – Simu ya Kipaumbele ya Madaktari

- madaktari wa familia na madaktari bingwa wanaweza kutumia wakalimani bila ya malipo, siku saba, masaa 24 kwa siku ili kuwasiliana nawe vyema
- madaktari wanaweza kupiga simu ya Kipaumbele 1300 131 450 ili kupata mkalimani kwa simu au kupanga mkalimani aje katika kituo ili kutafasiri. Unapaswa kuomba mkalimani wakati unapofanya miadi ili kurahisisha ziara yako.

### Kumlipa daktari

- madaktari wengine 'hulimbikiza malipo – bulk billing' kwa wagonjwa wao. Hii inamaanisha unapoenda kuonana na daktari wako hutoi malipo kwa vile serikali kuu humlipa daktari moja kwa moja kupitia kadi ya medicare.
- ikiwa daktari wako wa familia halimbikizi malipo, unamlipa, kisha unaendea kudai baadhi ya malipo hayo kutoka ofisi za medicare kwa kuonyesha risiti ya malipo. Hii inamaanisha kuwa utalipia tofauti ya malipo tuu.
- unaweza kulimbikiza malipo au kudai pesa kutoka kwa ofisi ya medicare kama una kadi ya medicare. Kwa habari kuhusu jinsi unavyoweza kupata kadi ya medicare, kama unastahili na orodha ya gharama piga simu 13 20 11 au tafuta kwa <http://www.medicareaustralia.gov.au/>.

### Miadi

- Fanya miadi mapema
- miadi huwa mifupi (dakika 10-15) lakini unaweza ukaomba miadi ya muda mrefu ikihitajikana wakati unaomba miadi
- usipofanya miadi, unaweza kuambiwa urudi wakati mwengine au usubiri kwa muda mrefu
- kila miadi ni ya mtu mmoja pekee
- kama hauwezi kuhudhuria miadi, unapaswa kumjulisha daktari wako ili uihairishe.
- unaweza kunufaika zaidi ikiwa utaandika mambo unayotaka kupata ushauri kabla ya kuenda kumwona daktari wako.
- mweleze daktari madawa yote unayotumia ukijumuisha madawa ya kienyeji, vitamini, miti shamba, n.k.
- mwonyeshe daktari madawa yote unayotumia.

Karatasi hii ya kweli iko katika mfululizo wa 10. idadi kamili:

1. Mfumo wa afya nchini Queensland
2. Kumwona daktari
3. Madawa
4. Hospitali za Queensland
5. Vituo vya afya ya jamii
6. Huduma za meno
7. Afya ya pamoja
8. Kuishi na afya na kuzuia magonjwa
9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu
10. Wewe na mfumo wa huduma ya afya

